Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

# ELIMU *Bulletin*

JARIDA LA MTANDAONI: *Toleo Na.38* - **2024**

wizara_elimuTanzania wizara_elimuTz www.facebook/moestvt.com www.wyestu.blogspot.com www.moe.go.tz ELIMUTZ




*Elimu Ujuzi Mwelekeo Mpya*

## Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023

## Sasa Rasmi



# SERIKALI

# Kuendelea kuwekeza katika sekta ya elimu

**- KAZI IENDELEE -**

# TAHARIRI

## Tanzania yajivunia mafanikio katika kutekeleza Elimu Jumuishi

Katika ulimwengu wa sasa unaozidi kuunganishwa na maendeleo ya haraka ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia, elimu imeendelea kuwa kiini muhimu cha maendeleo ya kila taifa.

Kwa zaidi ya miongo mitatu dhana ya elimu jumuishi imepata umaarufu mkubwa tangu ilipotambuliwa rasmi mnamo mwaka 1990.

Katika kutekeleza azma ya upatikanaji wa elimu kwa wote, Serikali ya Tanzania haikuachwa nyuma imekuwa ikifanya juhudi kuboresha miundombinu, kwa kuanzisha sera na program zinazolenga kuhakikisha Watoto wenye ulemavu na mahitaji maalum wanapata fursa ya elimu.

Mwaka huu Tanzania imeadhimisha miaka 30 ya utekelezaji wa elimu jumuishi, ni ukweli usiopingika Watanzania wameshuhudia maonesho mbalimbali ya kitaaluma, ubunifu na vipaji vya wenye mahitaji maalum lakini, tusisahau kutafakari, kujifunza, na kushiriki mafanikio tuliyofikia leo.

Tunaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuchukua hatua mbalimbali katika kutoa elimu bora, ikiwa ni pamoja na kutekeleza kwa vitendo mikataba mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, inaandaa Sera, miongozo na mikakati, lakini pia imeanza kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 Toleo la 2023 inayozingatia ujumuishwaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum katika elimu.

Aidha tunapongeza uboreshaji wa miundombinu ya ujifunzaji kwa wenye mahitaji maalum, ambapo mpaka sasa Serikali imefanikiwa kujenga mabweni 172, vyumba vya madarasa 44 na matundu ya vyoo 132 kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa shule za Msingi pamoja na kujenga shule 2 maalum za mfano ikiwemo Shule ya Sekondari Maalum Patandi.

Katika maadhimisho haya, ni wakati mzuri kwa jamii nzima kuungana na kuimarisha dhamira ya pamoja katika kusukuma mbele ajenda ya elimu jumuishi, tuunge mkono Serikali kuondoa vikwazo vinavyowazuia wanafunzi wenye mahitaji maalum kupata elimu bora.







BODI YA UHARIRI

Sylvia Lupembe
***Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini***

**Wachangiaji:**
Oliva Kato
Elizabeth Pancras
Veronica Chitunda
Nazareth Mwakabuta

**Mawasiliano:**
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya - Dodoma
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.
Simu: +255 26 296 3533

**Jarida hili linatolewa na**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Uwekezaji katika Elimu >

# Serikali kuendelea kuweka katika sekta ya elimu



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema kuwa Serikali inaendelea kupanua Mfuko wa Mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka bilioni 464 Mwaka 2020/21 hadi kufikia bilioni 787 Mwaka 2024/25.

Rais Samia ametoa kauli hiyo Septemba 27, 2024 baada kuzindua shule ya Sekondari ya Wasichana Samia Suluhu Hassan iliyopo Wilaya ya Namtumbo Mkoani Ruvuma, ambapo amewasisitiza wanafunzi kuhakikisha wanasoma kwa bidii na kutumia vizuri mifumo ya kitehama.

Shule ya Sekondari Samia Suluhu Hassan ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,200, na ni miongoni mwa Shule 26 za Wasichana za mchepuo wa Sayansi zinazojengwa Nchini kupitia Mradi wa SEQUIP unatekekezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Mohamed Mchengerwa amesema wanafunzi 4,843 wamekwisha ripoti kwenye Shule za Wasichana za Sayansi za Mikoa ambazo zimejengwa kwenye mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.

Waziri Mchengerwa amesema Sh. Bilioni 108 zimetolewa kwenye mikoa yote kwa ajili ya ujenzi wa shule hizo ambapo kila Mkoa umepata Sh. Bilioni 4.1 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu yote muhimu ya shule na baadhi kuongezewa Sh. Milioni 350 kwa ajili ya ukamilishaji wa bwalo.



Uwekezaji Elimu ya Juu >

# Njombe yajivunia kupata kampasi ya chuo kikuu



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda Septemba 20, 2024 amekagua maandalizi ya ujenzi wa Kampasi ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) inayojengwa Mkoani Njombe na Wizara kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET).

Wananchi wa Mkoa huo wajivua hatua ya kuanza kwa ujenzi wa Kampasi hiyo, ambao utaifanya Njombe kuwa na Taasisi ya kwanza ya Elimu ya Juu.

Mbunge wa Jimbo hilo Mhe. Deo Mwanyika amesema kuwa uamuzi wa Serikali kujenga Kampasi hiyo utasaidia na kuwakomboa wananchi wa mkoa huo kuwezesha kupata elimu ya Juu na kuhamasisha maendeleo nyanja mbalimbali za kijamii na kiuchumi.

Kwa Upande wake Makamu Mkuu wa Chuo - Taaluma, Prof. Razack Lokina amesema ujenzi wa Kampasi hiyo utaanza Disemba 2024, utagharimu shilingi bilioni 20 na kwamba ujenzi ukikamilika Chuo kinatarajiwa kuchukua wanafunzi 1,000.

Amesema Kampasi hiyo itaanza kutoa kozi za Stashahada na Shahada za ujuzi katika fani za Kilimo, TEHAMA, Misitu pamoja na mazao yake na zingine zinazoendana na shughuli za kiuchumi za Mkoa wa Njombe.



Utunzaji Vifaa vya Mafunzo >



# Prof. Nombo asisitiza utunzaji wa vifaa vya mafunzo VETA Kasulu

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo amekitaka Chuo cha Ufundi Stadi VETA Kasulu Mkoani Kigoma kutunza vifaa vilivyonunuliwa na Serikali kwa gharama kubwa ili viweze kutumika kwa muda mrefu katika kutoa mafunzo.

Prof. Nombo ametoa rai hiyo Septemba 10, 2024 alipotembelea Chuo hicho kukagua utekelezaji wa mafunzo, ambapo ameridhishwa na maendeleo ya Chuo hicho, ambacho mpaka sasa kimepokea wanafunzi zaidi ya 180 wa fani mbalimbali za muda mrefu na mfupi.

Aidha akiwa mkoani humo Prof. Nombo amewataka Wathibiti Ubora wa Shule Kigoma DC na Ujiji kufanya tathmini za kina shuleni kwa kuzingatia hali ya utekelezaji wa mtaala ulioboreshwa na mapendekezo ya utatuzi wa changamoto mbalimbali.

Nae Mkurugenzi wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi Dkt. Fredrick Salukele amewasisitiza Wathibiti Ubora kukagua pia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs) eneo la mtaala wa Sekondari na maadili.

Katika ziara hiyo Prof. Nombo aliambatana na Wawakilishi kutoka Ubalozi wa Canada Nchini Tanzania (Global Affairs Canada) Bi. Stephanie Brunet na Bi. Rasmata Barry kukagua utekelezaji Mradi wa Uwezeshaji Kupitia Ujuzi (ESP) unaotekelezwa Nchini na Jumuiya ya Vyuo na Taasisi za Ufundi Canada (CICan) katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDC).



# Uboreshaji Miundombinu >




# Waziri Prof. Mkenda aweka jiwe la msingi sekondari ya Makowo

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda Septemba 20, 2024 ameweka jiwe la Msingi la ujenzi wa shule ya Sekondari Makowo iliyopo katika Kata ya Makowo mkoani Njombe.

Akizungumza baada ya kuweka jiwe la msingi katika shule hiyo, Prof. Mkenda amewapongeza wakazi wa Kata hiyo kwa kuchangia na kuanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo kuchangia ujenzi wa shule, mabweni na vituo vya afya.

Aidha Waziri Mkenda amewahakikishia kwamba Serikali itaendelea kuunga mkono jitihada hizo za maendeleo ili kuimarisha utolewaji wa huduma bora kwa jamii.

Wananchi wa kata hiyo wameishukuru Serikali kwa ujenzi wa Shule ya kwanza ya Sekondari tangu uhuru ambayo imegharimu zaidi ya shilingi milioni 580 ndani ya miaka mitatu ya awamu ya sita.



Ubora ujenzi VETA >



# Kipanga asisitiza kuzingatia ubora ujenzi VETA Bunda



Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Mhe. Omari Kipanga amewataka Wahandisi wa ujenzi wa Chuo cha VETA cha Wilaya ya Bunda Mkoani Mara kuzingatia ubora wa kazi na ramani za majengo.

Kipanga ametoa rai hiyo Septemba 25, 2024 wakati akikagua ujenzi wa Chuo hicho ambacho ni miongoni mwa Vyuo 64 vinavyojengwa na Serikali baada ya maelekezo ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyesisitiza kuhakikisha kila wilaya ya Tanzania bara kinajengwa Chuo cha Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi cha Wilaya.

Amesema ujenzi wa Chuo cha VETA Bunda kinahusisha ujenzi wa majengo 18, yanayogharimu Shilingi milioni 324.5, na mpaka sasa tayari Serikali imeshatoa fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa Chuo hicho.

"Kukamilika kwa Chuo hiki kutasaidia kutoa elimu ya ujuzi kwa wakazi wa wilaya hii na jirani utakao wawezesha kujiajiri na kuajiriwa ili baadae waweze kutimiza ndoto zao" alisema Mhe. Kipanga.

Kwa upande wake Mkuu wa Chuo Bw. Hilary Majimbe amemshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya kwa kuendelea kuwekeza katika sekta ya Elimu na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kutekeleza maono ya serikali kwa vitendo katika kuandaa nguvu kazi yenye ujuzi.

Sera ya Elimu >

# Sera ya Elimu imewazingatia wanafunzi wenye mahitaji maalum - Dkt. Mahera






Serikali imeanza kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023, pamoja na Mitaala iliyoboreshwa kwa kuzingatia ujumuishwaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum ngazi zote za elimu.

Kauli hiyo imetolewa Septemba 20, 2024 jijini Arusha na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Wilson Mahera wakati akizungumza katika Kilele cha Maadhimisho ya Miaka 30 ya Elimu Jumuishi, ambapo amesema utekelezaji wa Sera hiyo pia unazingatia maadili, ujuzi, ubunifu na TEHAMA kwa wanafunzi wote.

"Tunajivunia mafanikio makubwa, tuna ongezeko la Wanafunzi walioandikishwa katika ngazi ya Awali, Msingi na Sekondari kutoka 3,789 mwaka 1997 hadi 97,305 mwaka 2024" alibainisha Mahera.

Vile vile Dkt. Mahera amesema kuwa walimu wa elimu maalum na jumuishi katika ngazi za Elimu Msingi wameongezeka kutoka 1,293 mwaka 1,997 kufikia 5,477 mwaka 2024.

Naibu Katibu Mkuu huyo ametoa wito kwa viongozi wa taasisi na wadau kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuhamasisha na kuchangia utekelezaji utoaji wa elimu kwa watu wenye mahitaji maalum.

Nae Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Elimu) Atupele Mwambene amesema Serikali itaendelea kusimamia zoezi la ubainishaji na kuhakikisha Watoto wenye mahitaji maalum wanaandikishwa shule na kupatiwa afua stahiki kulingana na mahitaji yao.

"Ofisi ya TAMISEMI itatekeleza kwa vitendo kuhakikisha wanafunzi wenye mahitaji maalum wanajengewa maadili mazuri kwa kuimarisha vituo vya malezi, ushauri na unasihi ili viweze kutoa huduma bora" Alisema Mwambene.

Mkurugenzi wa Elimu Maalum Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Magreth Matonya amesema Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 Toleo la 2023 imezingatia stahiki mbalimbali kwa wenye mahitaji Maalum kuhakikisha wanapata elimu bora kuchochea maendeleo yao.

Utekelezaji Elimu ya Lazima >




# Utekelezaji wa Elimu ya Lazima Miaka 10 kuanza mwaka 2027/28

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema kuwa utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023 kuhusu elimu ya lazima kuwa ya miaka 10 utaanza Mwaka 2027/28.

Prof. Mkenda amesema hayo Mkoani Ruvuma Septemba 26, 2024 wakati akizungumza katika Kongamano la Mafunzo kwa Umoja wa Wanawake Tanzania, ambapo ameongeza kuwa ifikapo Mwaka 2027/28 Mtoto ambaye hatakaa shuleni kwa miaka 10 hatua zitachukuliwa kwa mzazi au mlezi.

Waziri Mkenda ameongeza kuwa wahitimu wa Elimu ya Msingi ya miaka 6 watakutana na wahitimu wa mwisho wa elimu ya msingi ya miaka saba na wote wataanza kidato cha kwanza.

Aidha Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Caroylne Nombo amesema kuwa Wanafunzi wanaosoma Mkondo wa Amali watalazimika kusoma masoma matano ya lazima pamoja na somo moja la fani.



Prof. Nombo amesema kuwa mkondo huo una fani kuu 15, na kwamba masomo hayo ya lazima kuwa ni Hesabu, Kiingereza, Elimu ya Biashara, Lugha ya Mawasiliano, Hisitoria ya Tanzania na Maadili ambalo litafundishwa kwa kiswahili.

Katika Kongamano hilo Wizara imekabidhi nakala ya Vitabu vya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023 kwa Mwenyekiti wa UWT Bi. Mary Chatanda Mary Chatanda ili kusambaza kwa makundi mbalimbali.

Uwekezaji Elimu ya Sekondari >

# Milioni 961 za ujenzi wa Sekondari ya Mtapa zaondoa msongamano wa wanafunzi Igwachanya



Serikali imetumia zaidi ya shilingi milioni 961 kujenga shule ya Sekondari Mtapa iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe iliyojengwa kupitia Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Sekondari (SEQUIP).

Akizungumza baada ya kukagua ujenzi wa shule hiyo, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema kuwa Shule hiyo ni moja kati ya shule za Kata zinazojengwa nchini kwa lengo la kupunguza msongamano na wanafunzi kutembea umbali mrefu kufuata shule.

Prof. Mkenda ameongeza kuwa shule hiyo ni mwendelezo wa mpango wa serikali wa ujenzi wa shule mpya katika kata unaoendelea nchini na kwamba shule hizo zimewekewa miundombinu na maabara za kisasa ili kuwezesha wanafunzi kujifunza kwa nadharia na vitendo lakini pia zina maktaba na vyumba vya TEHAMA.

"Kinachoonekana hapa maabara za kisasa, maktaba na madarasa yaliyo bora utayakuta katika shule zote zinazojengwa nchi nzima. Sasa hivi wanafunzi wanasoma kwa vitendo na si nadharia pekee" amesisitiza Waziri huyo.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari Mtapa amesema kuwa uwepo wa shule hiyo umesaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi katika shule ya Sekondari Igwachanya.

Queen Mwenga Mwanafunzi wa Kidato cha tatu katika shule hiyo, amemshukuru Mhe. Samia Suluhu Hassan kwani kabla ya ujenzi huo wanafunzi walikuwa wakitembea mwendo mrefu na baadhi kukatisha masomo kutoka na kuchoka kutembea umbali mrefu kufuata shule.

Uria Mgaya Mwananchi wa Kata ya Igwachanya amesema kuwa shule hiyo imewapa amani wazazi kwani kwa sasa hawana wasiwasi watoto wao wanapokwenda shuleni kwani ipo karibu na kwamba watahakikisha wanalinda miundombinu ya shule hiyo ili iweze wasaidia vijana wengi wa kata hiyo.



# Uboreshaji Masomo ya Sayansi >

## Serikali kuongeza nguvu kwenye masomo ya sayansi - Mkenda





Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema kuwa hakuna Nchi Duniani inayoendelea bila Sayansi ya Teknolojia hivyo Serikali itaendelea kuongeza nguvu kwenye masomo ya Sayansi ili kupata wanafunzi walio bora kwa maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Prof. Mkenda amesema hayo Septemba 08, 2024 jijini Dar es Salaam akizungumza kwenye Marathon ya Bodi ya usajili wa Wahandisi Nchini, ambapo amesema kuwa kupitia Samia Skolashipu, Serikali inatoa mkopo wa asilimia miamoja kwa Wanafunzi waliofaulu vizuri masomo ya sayansi kidato cha Sita na kwenda Chuo Kikuu kusomea fani za Uhandisi, Tehama, Hisabati na Elimu tiba.

Lengo la mbio za ERB ni kuwainua na kuwawezesha wanafunzi wanaosoma masomo ya Sayansi na kuwezesha, Walimu wanaofundisha masomo ya Sayansi kwa Mkataba.

Huu ni msimu wa kwanza wa ERB Marathon na mbio hizi zitakuwa zinafanyika kila mwaka ifikapo mwezi wa tisa huku wakimbiaji mia saba na kuendelea wakialikwa kushiriki mbio hizi.

Waziri Mkenda ameweka historia ya aina yake kwa kuweza kumaliza kilomita kumi jambo ambalo limewafurahisha wanariadha wengi zaidi.

Mbio hizo zilianzia katika uwanja wa UDASA kupitia Samu Nujoma, Makomgo juu na mwisho ni katika viwanja vya UDASA vilivyopo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

# Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),**
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 6562,
7 Mtaa wa Magogoni,
11479 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2113694, 2113691
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

Mkurugenzi Mtendaji,
**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),**
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,
Barabara ya Mandela,
P.O. Box 76068,
15471 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 736 665 533/ 739 665 533
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

Katibu mtendaji,
**Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),**
Eneo la Viwanda Mikocheni,
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2624 au 32019,
14112 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET),**
S.L.P 17007, DODOMA.
Simu: +255 26 2323 121 / 0733 77 77 51
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),**
Nunge Street, Old Catholic Church Road,
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.
Simu: +255 23 244 0216
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),**
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P. 4302,
14113 Kijitonyama,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749
Baruapepe: dg@costech.or.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),**
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 0735 041168
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),**
S.L.P 34578,
Mikocheni B, Bima Road,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@tea.or.tz
dg@tea.or.tz

Mkurugenzi Mkuu
**VETA Makao Makuu,**
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
26 DODOMA.
Simu: +255 26 2963661
Baruapepe: info@veta.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)**
S.L.P 743,
23114 Engutoto, Block J, Plot No 216,
ARUSHA
Simu: +255 272 9700054
Barua Pepe:dg@taec.go.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),**
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu
16103 Dar es Salaam
Simu: +255222410700
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Ardhi University (ARU),**
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,
University Road,
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 738 357 310-12
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili (MUHAS),**
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,
Upanga Magharibi,
S.L.P. 65001,
11103 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2150302-6
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),**
S.L.P 3000,
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,
01 MOROGORO
Simu: +255 23 260511-4
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Mzumbe (MU),**
S.L.P 1, MOROGORO
Simu:
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz
info@mzumbe.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),**
S.L.P 259,
Mtaa wa Benjamin Mkapa,
Jengo la Benjamin Mkapa,
41107 DODOMA.
Simu: +255 26 2310001/2/3
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz
relations@udom.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),**
S.L.P. 23409,
14110 Open University Road,
Kinondoni Municipality,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2668820/ 2668992
Baruapepe: vc@out.ac.tz

RASI wa Chuo,
**Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),**
Taifa Road Next to Benjamin Willium,
S.L.P 2329,
15105 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2850975
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz
dpacademic@duce.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ushirika Moshi,**
06 Barabara ya Sokoine Moshi,
S.L.P 474
KILIMANJARO
Simu: +255 272 751 833
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),**
Mtaa wa Mkwawa Chuo,
S.L.P. 2513,
51111 IRINGA CBD.
Simu: +255 26 2702 751
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),**
S.L.P. 131,
Barabara ya 01 MUST,
01 MBEYA.
Simu: +255(0)25 2957542/4
Barua pepe: vc@mustnet.

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),**
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P. 447,
23301 TENGERU, ARUSHA
Simu +255 272970001
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere,**
S.L.P 976, Butiama, MARA
Simu:
Barua Pepe: info@mjnuat.ac.tz

Mkurugenzi
**Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),**
27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,
S.L.P 9283
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2150048/9
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Taifa ya UNESCO,**
7 Magogoni Street,
P. O. Box 20384,
11479 DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292
Baruapepe: info@natcom.go.tz

Mkurugenzi,
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,
S.L.P. 20679,
11103 DAR ES SALAAM
Simu:
Baruapepe: info@iae.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ufundi Arusha (ATC),**
Junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,
P.O. Box 296,
23105 ARUSHA.
Simu: +255 (0) 27-297 0056
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

Mkurugenzi,
**Kituo cha Maendeleo Dakawa,**
S.L.P 1733,
MOROGORO.

Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),**
Kona ya Bibi Titi na Barabara ya Morogoro
S.L.P 2958
11104 DAR ES SALAAM
Simu:
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),**
30 Barabara ya Kibada,
S.L.P 9193,
17107 Kigamboni,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz